



# Takwimu za ulemavu katika shule zilizo kwenye mazingira magumu ya kibinadamu

Utafiti uliyofanyawa Uganda unaashiria nini?



## Muktadha wa utafiti

Ripoti ya Dunia ya Ulemavu inakadiria kuwa hadi 15% ya idadi ya watu wana ulemavu, ingawa ukusanyaji wa takwimu sahihi za ulemavu bado ni changamoto. Mara nyinyi ni ghali na si sahihi. Pengo hili la takwimu Linawagusa hasa watoto na vijana walio na ulemavu, na kuwafanya "wasiweze kuonekana kisiasa na kijamii," na piahuweka vizuizi kwao kupata huduma muhimu kama elimu na afya.

Kuchagua zanasahihi ya ukusanyaji wa data ni moja wapo ya changamoto kubwa katika ukusanyaji wa takwimu za ulemavu.

Hati hii inaelezea matokeo ya utafiti unaoteklezwa na Humanity & Inclusion na kufadhiliwa na Education Cannot Wait. Utafiti huulichunguza uthabiti wa Toleo la Walimu wa Mtoto (CFM-TV) na matokeo ya elimu jumuishi katika mazingira magumu.

## Utafiti huo ulifanywa vipi?

Kipindi cha mradi: 2022 - 2023

**Mahali/Eneo:** Kyaka II, Wilaya ya Kyegegwa, Uganda

**Walengwa:** Walimu na wanafunzi katika shule za msingi za umma

**Mbinu/Methodolojia:** Mbinu mchanganyiko kulingana na mahojiano ya utambuzi na walimu, ikifuatiwa na tafiti za kiasi kulinganisha tathmini mbili zilizofanywa na walimu sawa wiki 3 tofauti na kulinganisha tathmini za walimu na walezi; na kuzingatia majadiliano ya kikundi na walimu

## Kuhusu CFM-TV

**Mhojiwa:** Waalimu

**Wanafunzi:** watoto wa umri wa miaka 5 hadi 17

Maswali 13

**Vigezo/vipengele 12:** kuona, kusikia, kutembea, mawasiliano, kujifunza, kukumbuka, kuzingatia, kukubali mabadiliko, kudhibiti tabia, kupata marafiki, wasiwasni na unyongofu/huzuni/simanzi

**Uchambuzi:** watoto wanatambuliwa kuwa na ugumu wa utendaji ikiwa "wanapata ugumu mwingu" au "hawawezi kufanya kabisa" katika angalau ya kitendo/kipengele/kigezo kimoja

## Matokeo muhimu

- Tathmini ya walimu baada ya wiki 3 ilionesa kiwango cha wastani cha uthabiti. Walimu kama wawakilishi walitoa takwimu za ulemavu za kuaminika
- Idadi ya wanafunzi darasani na wakati wa kipindi shuleni hazikuwa na athari yoyote kwa uwezo na motisha ya waalimu ya kutathmini wanafunzi

- Matokeo ya waalimu na walezi yalionyesha kiwango duni cha uwiano
- Utafiti huu unabaini kuwa utambuzi wa ulemavu huwa kwa njia mbalimbali na hulingana na mitazamo ya kipekee ya walezi na waalimu kuhusu ulemavu.

## Manufaa ambayo hayakutarajiwa kwa waalimu na wanafunzi

Tathmini ya CFM-TV na waalimu



Waalimu kutambua mahitaji ya watoto



Waalimu kuwa na uangalifu chanya na mabadiliko mazuri, shughuli za ujumuishi zaidi



Watoto kuwa na muitikio/mabadiliko chanya na kupungua kiwango cha utoro



Hisia ya kuwa mamaja ("darasa langu") na ongezeko la ushirikishwaji kwa wanafunzi wote darasani



## Athari kwa wadau wa elimu na watendaji

- Zanakutumika mashulenii kwa madhumuni ya elimu.
- Kuwa na zana nzuri na thabitiza kuzalisha takwimu juu ya watoto walio na ugumu katika utendaji zinaweza kuchangia kuboresha masomo katika mazingira magumu ya kibinadamu: kuboresha ufundishajikwa waalimu; kufuatilia mahudhurio ya watoto wenye changamoto ya utendaji shuleni; kusambaza ujumbe kitaifa na kimataifa.
- Utafiti zaidi bado unahitajika, hasa kuelewa vizuri mabadiliko yaliyosababishwa na matumizi ya CFM-TV kwa mwalimu na darasani.

Kujua zaidi kuhusu utafiti huu:

[www.hi.org/en/disability-data-in-schools-in-emergency-and-protracted-crisis](http://www.hi.org/en/disability-data-in-schools-in-emergency-and-protracted-crisis)

Mtafiti mkuu: Aude Brus (a.brus@hi.org)



Utafiti na Mafunzo